JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

Namba za simu SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASONYA,
S.L.P 159,
Mkuu wa shule: **0755551641/0627675919** **TUNDURU – RUVUMA**.
Makamu Mkuu wa Shule: **0757350293** 23.05.2018.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……..
…….
S.L.P ……
……..

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASONYA, HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU, MKOA WA RUVUMA MWAKA 2018/2019.

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha Tano katika shule ya sekondari ya wasichana Masonya tahasusi ya ……. mwaka 2018.
Aidha natumia nafasi hii kukupongeza kwa kufaulu vizuri mitihani yako yaTaifa ya kumaliza elimu ya kidato cha nne.
Shule ya Sekondari Masonya ni ya bweni. Shule hii ipo umbali wa kilometa 12 Kaskazini mwa mji waTunduru. Kilometa sita (6) ukitoka Tunduru mjini kuelekea barabara kuu iendayo Songea, upande wakulia utaona kibao kinaonesha shule ilipo. Kutoka kwenye kibao hicho ni umbali wa km 6 mpaka shuleni. Kila mwanafunzi atajitegemea kwa safari zote za kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo au dharura yoyote ile.
Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo:

1. Maelezo ya kujiunga na kidato cha Tano 2018 (Joining Instruction)
2. Fomu ya kupimwa Afya hospitali na Mganga Mkuu wa Wilaya/Kituo cha Afya (Medical examination report form)
3. Fomu ya kukubali/kukataa nafasi ya kujiunga na shule hii pamoja na ahadi ya Mzazi/Mlezi kulipa karo na michango ya shule.
4. Fomu ya Taarifa binafsi ya Mwanafunzi.

Kumbuka kuwa kila mwanafunzi anapaswa kujaza fomu zote husika kwa ukamilifu na kuzirejesha hapa shuleni siku atakaporipoti.
Usafiri wa kutoka mjini mpaka shuleni ni Bajaji/Pikipiki (bodaboda) unapatikana katika kituo cha mabasiTunduru Mjini nauli ni shilingi za kitanzania 5,000/= kwa bodaboda na 8,000/= kwa bajaji.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 02/07/2018. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo bila kuchelewa.

KARIBU SANA MASONYA SEKONDARI!

ELICE O. BANDA.
MKUU WA SHULE

1. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

1.1 Sare ya shule ni kama ifuatavyo

a. Sketi mbili (2) rangi ya kijivu ya kupauka,(***kitambaa cha suti***) **ndefu zinazokaribia usawa wa kisigino** mshono Rinda box.

b. Gauni mbili (2) (shamba dress) rangi ya bluu, (***kitambaa aina ya polista***) ziwe **ndefu zinazokaribia usawa wa kisigino** mshono wa solo mikono mifupi .

c. Skafu mbili (2) za rangi ya kijivu.

d. Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi

e. Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba (jozi mbili)

f. Soksi nyeupe jozi mbili (2) (stockings)

g. Sweta moja ya kijivu (iwe na rangi moja tu)

h. Unaruhusiwa kushona Hijab kwa anayetaka. Hivyo Hijab ishonwe nyumbani nusu kanzu na inayovuka makalio, na isifunike viganja vya mikono(kitambaa aina ya haluwa).

i. Tracksuti moja yenye rangi ya bluu bahari (light blue) kwa ajili ya michezo na wakati wa usiku kuzuia mbu darasani.

1.2 Ada na michango ya shule

a. Ada ya shule (karo) Tshs. 70,000/= kwa mwaka. Mwanafunzi hatapokelewa kama hatalipa walau nusu ya Ada ya mwaka mzima, yaani Tshs 35,000/=. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. **70901100056-(Jina la Akaunti ni shule ya sekondari Masonya. Katika bank ya NMB** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

b. **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni :-**

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani kwa mwaka.
ii. Shilingi 6,000/=kwa ajili ya kitambulisho na picha.
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma kwa mwaka.
iv. Shilingi 30,000/=kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi, na vibarua wengine kwa mwaka.
v. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya Huduma ya kwanza kwa mwaka.
vi. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa).

Jumla ya michango yote na ada ni Tshs 156,000/= (laki moja na elfu hamsini na sita tu kwa mwaka.)

- **Ada na michango yote ilipwe katika Bank ya NMB, Akaunti Na. 70901100056- (Jina la Akaunti ni shule ya sekondari Masonya)**

c. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Ream moja (01) A4 ya karatasi (kwa mwaka)

ii. Godoro moja lenye ukubwa wa Ft 2½ kwa 6.

iii. Shuka mbili (2) rangi ya bluu bahari na blanketi moja na chandarua moja.

iv. Counter book kubwa zakutosha, kalamu za kuandikia (peni),kalamu za risasi, begi la kubebea daftari na rula.

v. Mkebe (Mathematical set).

vi. Scientific calculator kwa wanaosoma Geography.

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli,kikombe na kijiko.

viii. Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko ujazo wa lita 10 kwa kila moja.

ix. Jembe moja(01), Panga au Fyekeo moja (01), Fagio la plastiki moja (01), Fagio la chelewa moja (01), na Reki moja (01).

D. VIFAA VINGINEVYO

i. Sanduku la bati kwa ajili ya kuwekea nguo na vifaa vingine.

ii. Taulo na ndala kwa ajili ya kuogea.

iii. Picha nne (04) ndogo za wazazi, na ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi pamoja na namba zao za simu.

NB. (i)Maso*nya ni eneo lenye mbu wakali na malaria hivyo chandarua ni muhimu.*

(ii)Huruhusiwi kusuka nywele hivyo unatakiwa kuwa na nywele fupi.

2. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa (utoro)
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mewanafunzi/kumpiga mwalimu au mtu yoyote 3ule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigra na bangi
ix. Uasharati, uhusiano wa jinsi moja kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba ndani na nje ya shule,
xi. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.

xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua au kuhatarisha maisha ya watu wengine.
xvi. Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi.

HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASONYA

A: SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi ..... ninakubali kujiunga kidato cha..... katika shule ya sekondari ya wasichana (Bweni) Masonya.
2. Ninaahidi kufika shuleni tarehe ..... iliyopangwa bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitakuwa mwanafunzi bora mwenye bidii na utii kwa sheria za shule, walimu, walezi na viongozi wa shule kwa muda wote nitakapokuwepo shuleni.
3. Pia ninaahidi kutoshiriki katika migomo yeyote,kufanya fujo, au makosa yeyote ya jinai kwa kipindi chote nitakachokuwa shuleni.

   SAINI .....

   TAREHE .....

B: SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

1. Mimi.....ninakubali/sikubali mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari ya wasicha ya Masonya kuanzia tarehe .....
2. Ninaahidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kufika navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya maagizo (Joining Instruction).
3. Nitahakikisha kwamba mtoto wangu amesoma sheria zote muhimu za shule na kuzielewa, na ameahidi mbele yangu kuwa atakuwa mtiifu na mwenye bidii (darasani na nje ya darasa)
4. Ninaahidi sitamsumbua mkuu wa shule wala viongozi wengine wa serikali kwa kuomba uhamisho wa mtoto wangu kwenda sekondari nyingine bila sababu ya msingi.
5. Ninaahidi mtoto wangu hatajihusisha na migomo, fujo au vitendo vya uvunjifu wa amani awapo shuleni.
6. Awapo shuleni mtoto wangu alelewe katika dini ya .....
7. Anuani yangu ya kudumu ni:.....
8. Namba ya simu: .....

SAINI..... TAREHE.....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA MASONYA

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili .....
2. Tarehe ya kuzaliwa ..... (tarehe,mwezi,mwaka)
3. Kabila ..... Taifa .....
4. Dini ..... Dhehebu .....
5. Jina la Baba ..... Taifa .....
6. Anuani ya Baba ..... Simu na .....
7. Kazi ya Baba .....
8. Jina la Mama .....
9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana
   .....
10. (a) Jina na anuani ya mlezi (kama si mzazi)
    .....
    (b) Kama mzazi ni mlezi uhusiano wako naye
    .....
11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi (Taja sehemu moja tu utakayokwenda kila wakati na anuani)
    .....
12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi.

Saini ya Mwanafunzi ..... Tarehe .....

Saini ya Mzazi/Mlezi ..... Tarehe .....

TUNDURU DISTRICT COUNCIL
MASONYA SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX **159,**
TUNDURU.
DATE: ……

THE MEDICAL OFFICE
……
……
……

STUDENTS' FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a Medical Officer in respect of all pupils from this school

1. Full pupils name ……
2. Age …….. (Years)……
3. Food counts (Red and white) …… ……
4. Stool Examination ……
5. Urinalysis ……
6. Syphilis tests ……
7. Venereal disease test ……
8. T.B Test……
9. Eye Test……
10. Ear ……
11. Chest ……
12. Spleen ……
13. Abdomen ……
14. Urine for plan test ……

ADDITIONAL INFORMATION (*If any*) e.g. Physical affects or impairment(s) arm, leg, Infections chronic family disease etc.

……
……

I certify that the above is fit/unfit to pursue educators as stated above.

Signature ……
Designation ……
Station ……
Date ……